# Marudisho ya Kodi ya Mapato

# EITC

*Pata pesa za ziada mfukoni*

Marudisho ya kodi ya mapato (EITC au EIC) ni malipo ya kodi yanayoweza kurejeshwa kwa ajili ya watu binafsi na wanandoa wenye mapato ya chini hadi ya wastani, hasa wale walio na watoto. **Huenda ukastahiki (TAZAMA MIONGOZO HAPA CHINI)!**

**Marudisho ya Kodi ya Mapato (Earned Income Tax Credit, EITC) ya hadi**

## $8,046

kiwa uliishi na **watoto watatu au zaidi** katika mwaka wa 2025 na familia **yako ilipata mapato ya juu zaidi ya $61,555 (au mapato ya juu zaidi ya $68,675 kwa wafanyakazi waliofunga ndoa),** basi unaweza kupata kiasi cha hadi **$8,046.**

**Marudisho ya Kodi ya Mapato (Earned Income Tax Credit, EITC) ya hadi**

## $7,152

Ikiwa uliishi na **watoto wawili** katika mwaka wa 2025 na familia **yako ilipata mapato ya juu zaidi ya $57,310 (au mapato ya juu zaidi ya $64,430 kwa wafanyakazi waliofunga ndoa),** basi unaweza kupata kiasi cha hadi **$7,152.**

**Marudisho ya Kodi ya Mapato (Earned Income Tax Credit, EITC) ya hadi**

## $4,328

Ikiwa uliishi na **mtoto mmoja** katika mwaka wa 2025 na familia **yako ilipata mapato ya juu zaidi ya $50,434 (au mapato ya juu zaidi ya $57,554 kwa wafanyakazi waliofunga ndoa),** basi unaweza kupata kiasi cha hadi **$4,328.**

**Marudisho ya Kodi ya Mapato (Earned Income Tax Credit, EITC) ya hadi**

## $649

Ikiwa **hukuwa na watoto walioishi nawe katika mwaka wa** 2025 na ulipata **mapato ya juu zaidi ya $19,104 (au mapato ya juu zaidi ya $26,214 kwa wafanyakazi waliofunga ndoa),** na ulikuwa na umri wa kati ya miaka 25 na 64, unaweza kupata kiasi cha hadi **$649.**

**Unahitaji Msaada wa Kurejesha Kodi?** Msaada wa kurejesha kodi bila malipo unapatikana kwa familia zinazostahiki kupata Marudisho ya Kodi ya Mapato (Earned Income Tax Credit, EITC) **Geuza kipeperushi ili uone orodha ya mashirika yanayoweza kukusaidia kurejesha kodi yako.**

DAYTON

## Pata Msaada wa Kurejesha Kodi Yako Bila Malipo! Utarejeshewa Pesa Haraka, Bila Ada Zozote!

Wafanyakazi wa kujitolea waliopokea mafunzo kutoka kwa Huduma ya Mapato ya Ndani (Internal Revenue Service, IRS) wanapatikana ili kusaidia wafanyakazi wanaostahiki kupata Marudisho ya Kodi ya Mapato (Earned Income Tax Credit, EITC) kujaza fomu zao za kurejesha kodi bila malipo. Maeneo ya Msaada wa Kurejesha Kodi ya Mapato Kutoka kwa Wafanyakazi wa Kujitolea **(Volunteer Income Tax Assistance, VITA) yatafunguliwa kuanzia Januari 24 hadi Aprili 15.**

**Maeneo yafuatayo yaliyoidhinishwa na Huduma ya Mapato ya Ndani (Internal Revenue Service, IRS) ni wanachama wa Muungano wa Dayton wa Marudisho ya Kodi ya Mapato (Earned Income Tax Credit, EITC) na yako katika eneo la Dayton. Piga simu kabla ya kutembelea maeneo hayo ili kupanga miadi:**

**Beavercreek Senior Center**
789 Orchard Lane • 45432
937-426-6166 ♿

**Fairborn Senior Center**
325 N. Third Street • 45324
937-878-4141 ♿

**Greene County Xenia Library**
76 E. Market Street • 45385
937-352-4000 ♿

**The Job Center**
1133 Edwin C. Moses Blvd. • 45417
937-913-2000 ♿

**Miamisburg Community Center**
305 Central Avenue • 45342
937-866-8999 ♿

**Northwest Branch Library**
2410 Philadelphia Drive • 45406
937-913-2000 ♿

**Partners In Hope**
180 E Race Street • 45373
937-335-0448 ♿

**Trotwood Branch Library**
855 E Main Street • 45426
937-913-2000 ♿

**St. Paul United Methodist Church**
101 Huffman Avenue • 45403
937-252-4467 ♿

♿ Inaonyesha kwamba eneo hilo linaweza kufikiwa na watu wanaotumia viti vya magurudumu

**Kwa maelezo kuhusu maeneo mengine ya kurejeshea kodi BILA MALIPO katika eneo la Dayton, piga simu kupitia 937-913-2000**

## Sharti ubebe vitu vifuatavyo unapokuja kwenye maeneo ya kurejeshea kodi:

- Kitambulisho chenye picha
- Fomu za W-2 za mapato ya mwaka wa 2025
- Kadi za Usalama wa Jamii (Social Security, S.S.) au Nambari za Utambulisho za Mlipa Kodi Binafsi (Individual Taxpayer Identification Numbers, ITIN) kwa ajili yako wewe na watu wote wa familia yako walioongezwa katika marejesho yako ya kodi
- Ikiwa ulikuwa na gharama za Utunzaji wa Watoto katika mwaka wa 2025, leta nambari ya Usalama wa Jamii (Social Security, S.S.) ya Mtoa Huduma au Nambari ya Kitambulisho cha Mwajiri (Employer ID Number, EIN) na anwani. Pia beba hati za malipo za jumla ya pesa ulizomlipa Mtoa Huduma, na kiasi ulicholipia kila mtoto.
- Barua zozote ulizopokea kutoka kwa Huduma ya Mapato ya Ndani (Internal Revenue Service, IRS) katika mwaka wa 2025 pamoja na fomu za 1098 na 1099 (kama zipo)
- Ikiwa ungependa pesa utakazorudishiwa ziwekwe moja kwa moja katika akaunti yako ya akiba na/au ya pesa za matumizi, leta nambari za akaunti zako unapokuja kwenye eneo la kufanyia marejesho ya kodi.
- Ikiwa una mume/mke na mnafanya marejesho ya kodi kwa pamoja, sharti kila mmoja wenu awepo ili kuchakata marejesho ya kodi.

**Kwa Maelezo Zaidi:**
**Piga Simu kwa Huduma ya Msaada ya United Way of the Greater Dayton Area Kupitia 913-2000**